Zana ya Kadi Rahisi ya Kadirio la Umaskini Kenya

Mark Schreiner

31 Juni 2018

This document is in English at scorocs.com
Maandīko maya meho kwa rūthiomi rwa Gīkūyū rūredainī rwa scorocs.com
Andika ni ondik kod Dholuo e scorocs.com
Ũandĩki ũũ nĩ wa Kĩkamba mũtandaonĩ scorocs.com
Amangana aya ase omonwa bwe'Ekegusii ase scorocs.com
Maandiko yaa yari na mugambo jwa Kimiru kiri scorocs.com
Sirutik chuto komiten en Kalenjin en scorocs.com
Waraka huu ipo kwa lugha ya Kiswahili kwenye scorocs.com

Muhtasari

Zana ya kutathmini umaskini ya Kadi Rahisi ya Kadirio la Umaskini (*Scorocs™ Simple Poverty Scorecard®-brand poverty-assessment tool*) ya nchi ya Kenya ni mbinu nafuu, na wazi ya kutumiwa na miradi ya kuwasaidia maskini kuthibitisha na kuboresha utendakazi wa kijamii kwa kupata kujua hali ya uchumi wa kijamii ya washiriki wao. Majibu ya viashiria 10 vya kadi ya kadirio yanaweza kukusanywa kwa takriban dakika 10 na kisha kutumika kukadiria viwango vya umaskini kulingana na matumizi, kufuatilia mabadiliko katika viwango vya umaskini, au kuwapanga washiriki kwa makundi kwa ajili ya shughuli tofauti.

Dokezo la toleo

Kadi hii mpya ya kadirio ina msingi kwenye data kutoka mwaka wa 2015/16. Inapaswa kutumika kuanzia sasa kuendelea mbele, na inachukua nafasi ya kadi ya zamani ya kadirio ya Kenya ambayo inatumia data kutoka mwaka wa 2005/6. Katika matarajio ambayo—yakikosa kubadilika—yanawezesha makadirio ya mabadiliko katika viwango vya umaskini baada ya muda, ulinganishaji makadirio kati ya kadi hizi mbili za kadirio kwa tahadhari yanawezekana kwa mstari wa umaskini wa chakula na kwa mistari mingine ya kitaifa ya umaskini (si kwa mistari mingine).

Shukrani

Data zimetoka kwenye Kenya National Bureau of Statistics. Shukrani kwa Paul Kemboi Samoei na Rose Mungai. Translated by SwahiliSpace, info@swahilispace.com.

Legal: "Scorocs" and "Prove and improve the good you do" are Trademarks (and "Simple Poverty Scorecard" is a Registered Trademark) of Scorocs, L.L.C. for its brand of poverty-assessment tools. Copyright © 2018 Scorocs.

Scorocs™ Simple Poverty Scorecard® Tool

			Name	Identifier
Interview ID:				
Interview date:		Participant:		
Country:	KEN	Field agent:		
Scorecard:	003	Service point:		
Sampling wgt.:		Number of household members:		

Indicator	Response	Score
1. Kuna jamaa wa kaya wangapi?	A. Wanane au zaidi	0
	B. Wasaba	3
	C. Wasita	6
	D. Watano	10
	E. Wanne	14
	F. Watatu	21
	G. Wawili	25
	H. Mmoja	34
2. Je, ni jamaa wa kaya wangapi wana simu ya mkononi?	A. Hakuna	0
	B. Mmoja	6
	C. Wawili au zaidi	10
3. Je, kuna jamaa yeyote wa kaya ambaye ana ulemavu ambao humzuia kujihusisha na shughuli ya kiuchumi?	A. Ndiyo	0
	B. La	4
4. Katika siku 7 zilizopita, je, kuna jamaa yeyote wa kaya aliyefanya kazi kwa angalau saa moja wao binafsi au kama mwajiriwa katika kampuni ya kibiashara, kwa mfano, kama mfanyabiashara, muuzaji duka, kinyozi, fundi wa nguo, fundi wa mbao, dereva wa teksi, mwoshaji magari, na kadhalika?	A. La	0
	B. Ndiyo	2
5. Katika siku 7 zilizopita, je, kuna jamaa yeyote wa kaya alikuwa mfanyakazi ambaye hajaajiriwa rasmi katika kazi yake kuu/msingi?	A. Ndiyo	0
	B. La	5
6. Je, kiongozi/mwanandoa wa kiume anaweza kusoma na kuandika kwa lugha yoyote?	A. La	0
	B. Hakuna kiongozi/mwanandoa wa kiume	2
	C. Ndiyo	3
7. Je, kiongozi/mwanandoa wa kike (aliye na umri wa juu zaidi) amefikia kiwango gani cha juu zaidi cha elimu, na ni darasa lipi la juu zaidi alilokamilisha katika kiwango hicho?	A. Hakuna, madrassa/*duksi*, chekechea, shule ya msingi darasa la 1, au nyingine	0
	B. Shule ya msingi darasa la 2 hadi 6	4
	B. Shule ya msingi darasa la 7 au 8	7
	D. Hakuna kiongozi/mwanandoa wa kike	8
	E. Shule ya upili kidato cha 1 hadi 3	10
	E. Shule ya upili kidato cha 4, au zaidi	16
8. Je, kaya hii inatumia vyumba vingapi kuishi (usihesabu bafu, vyoo, ghala, wala gereji)?	A. Kimoja, au hakuna	0
	B. Viwili	5
	C. Vitatu	8
	D. Vinne au zaidi	12
9. Je, ni nyenzo gani kuu iliyotumiwa kujenga kuta za nyumba kuu?	A. Vijiti, matope/samadi, nyasi/mafunjo, hakuna kuta, au nyingine	0
	B. Mabati, plaiwudi, kadibodi, au mbao zilizotumika	1
	C. Mwanzi pamoja na matope, mawe pamoja na matope, matofali ya udongo na nyasi ambayo hayajafunikwa, matofali ya udongo na nyasi yaliyofunikwa, mawe na saruji, saruji, matofali, mawe ya saruji, au mbao	5
10. Je, kaya ina televisheni inayofanya kazi?	A. La	0
	B. Ndiyo	9

Copyright © 2018 Scorocs.
Score:

Karatasi ya Ukurasa wa Nyuma: Jamaa wa Kaya, Umri, Simu za Mkononi, Ulemavu, na Hali ya Kazi

Jaza kichwa cha kadi ya kadirio kwanza. Jumuisha kitambulishi cha kipekee cha mahojiano (ikiwa kinajulikana), tarehe ya mahojiano, na sampuli ya uzito wa mshiriki (ikiwa unajulikana). Kisha rekodi jina kamili na nambari ya utambulisho ya kipekee ya mshiriki huyo (ambaye huenda akawa ni tofauti na anayejibu), ya ajenti wa nyanjani wa mshiriki (ambaye huenda akawa tofauti na mhoji), na ya kituo cha huduma ambacho mshiriki hutumia.

Kisha umsomee anayejibu: *Tafadhali nieleze majina ya kwanza (au majina ya utani) na umri wa jamaa wote wa kaya yako, ukianzia na kiongozi.* Kaya *ni mtu au kundi la watu (bila kujali uhusiano wa damu au ndoa) ambao wanaishi katika boma moja (yenye ua au bila ua) ambao wako chini ya kiongozi mmoja, na ambao wana chanzo sawia cha chakula na/au pato kama kitu kimoja jinsi kwamba wana mipango sawia ya kutunza makazi yao (yaani, wanatumia au wanategemea bajeti moja).*

Andika jina la kwanza/jina la utani na umri wa kila jamaa kulingana na miaka kamili aliyohitimu. Unahitajika kujua umri hasa wa jamaa ikiwa tu huenda ukawa umekaribia 6. Weka alama ni nani ambaye ni kiongozi/mwanandoa wa kiume (ikiwa yupo) na ni nani ambaye ni kiongozi/mwanandoa wa kike (mwenye umri wa juu zaidi) (ikiwa yupo). Rekodi idadi ya jamaa wa kaya kwenye kichwa cha kadi ya kadirio karibu na “Number of household members:”. Kisha uweke mduara kwenye jibu la kiashiria cha kwanza cha kadi ya kadirio kinachohusu ukubwa wa kaya.

Kwa kila jamaa wa kaya, uliza kama jamaa huyo ana simu ya mkononi. Weka alama kwenye jibu linalolingana la kiashiria cha pili kuhusu simu za mkononi.

Kwa nia sawia, uliza kila jamaa kama yeye ni mlemavu, na uweke alama kwenye jibu la kiashiria cha tatu kuhusu ulemavu.

Kisha umwulize kila jamaa ambaye ana umri wa miaka 6 au zaidi kuhusu kazi yake binafsi (au umiliki wa biashara) kando na ukulima, na uweke alama kwenye jibu la kiashiria cha nne.

Mwishowe, mwulize kila jamaa wa kaya kuhusu kazi ya kawaida, na uweke alama kwenye jibu la kiashiria cha tano. Kisha usome maswali tano yaliyosalia kwa sauti, na kuweka alama kwenye majibu.

Kila wakati kumbuka na utumie maagizo ya kina yaliyo kwenye “Interview Guide”.

Jina la kwanza au jina la utan	**Umri**	**Kiongozi au mwanandoa wa kiongozi?**	**Je, [JINA] ana simu ya mkononi?**	**Je, [JINA] ana ulemavu ambao humzuia kujihusisha na shughuli ya kiuchumi?**	**Ikiwa [JINA] ana umri wa miaka 6 au zaidi, basi katika siku 7 zilizopita, je, aliyefanya kazi kwa angalau saa moja yeye binafsi au kama mwajiriwa katika kampun ya kibiashara, kwa mfano, kama mfanyabiashara, muuzaji duka, kinyozi, fundi wa nguo, fundi wa mbao, dereva wa teksi, mwoshaji magari, na kadhalika?**	**Ikiwa [JINA] ana umri wa miaka 6 au zaidi, basi katika siku 7 zilizopita, je, alifanya kazi katika ajira yake kuu/msingi kama mfanyakazi ambaye hajaajiriwa rasmi?**
1.		Kiongozi (kiume) Kiongozi (kike)	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
2.		Mwanandoa (kiume) Mwanandoa (kike) Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
3.		Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
4.		Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
5.		Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
6.		Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
7.		Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
8.		Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
9.		Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
10.		Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
11.		Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
12.		Mwingine	La Ndiyo	La Ndiyo	<6 au mlemavu La Ndiyo	<6, mlemavu, au hakufanya kazi La Ndiyo
Idadi ya jamaa:		—	**# Ndiyo:**	**Yoyote ‘ndiyo’?**	**Yoyote ‘ndiyo’?**	**Yoyote ‘ndiyo’?**